



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



TANGAZO LA ZABUNI

SIMU NA: 026 2782111 (DED)
FAX NA: 026 2782857 (DED)
Barua pepe: ded@njombedc.go.tz

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,
S. L. P. 547,
NJOMBE

Tarehe: 29/05/2023

KWA AJILI YA: UTOAJI WA HUDUMA YA ULINZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

ZABUNI Na. LGA/031/2023/2024/HQ/NCS/01

1. Mwaliko huu wa zabuni unafuatia Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inatoa mwaliko wa zabuni ya huduma ya ulinzi kwa kampuni zote zenye sifa ya utoaji wa huduma ya Ulinzi kuanzia mwezi Julai 1, 2023 kwa mkataba ambao utatolewa na mwaliko wa zabuni hii.
3. Eneo la utoaji huduma litakuwa ni katika **Majengo na ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.**
4. Mtoa huduma (MH) lazima akidhi vigezo vifuatavyo:-
 - (i) Mtoa Huduma awe na vibarua wa ulinzi wa kutosha kufanya kazi ya ulinzi na atapaswa kuambatanisha orodha ya majina ya vibarua hao.
 - (ii) Mtoa huduma awe ni mmiliki au mwakilishi wa kampuni husika ya utoaji huduma ya ulinzi na sio dalali wa kampuni.
 - (iii) Orodha ya mikataba ya ulinzi ambayo mtoa huduma amewahi kufanya hivi karibuni inayofanana na huduma hii **isiyopungua miwili. Mtoa huduma lazima aonyeshe majina na anuani ya mwajiri aliyempa kazi hiyo kwa ajili ya uthibitisho.**
5. Kampuni zenye sifa na uwezo wa kutoa huduma za ulinzi wanakaribishwa kufika katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliyopo Njombe Mjini karibu na NMB na Tanesco barabara ya Songea ili kuchukua kotesheni ya zabuni na mchanganuo wa kazi hii ya ulinzi. Mwombaji atalipia kiasi cha Tsh. 20,000/= (elfu ishirini tu) wakati wa kuchukua kotesheni.

Barabara ya Njombe - Makambako (Kata ya Mtwango Kijiji cha Lunguya), SLP 547 Njombe, Simu: +255 26 2782111 (Mkurugenzi), +255 26 2782027 (Maulizo), Nukushi +255 26 2782857 Barua pepe: info@njombedc.go.tz; Tovuti: www.njombedc.go.tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



6. Mwombaji atatakiwa kujaza na kuwalisha mchanganuo wa gharama ya Huduma ya Ulinzi kulingana na mahitaji ya Halmashauri.
7. Mwisho wa kuwasilisha kotesheni ni **Alhamis tarehe 01 Juni, 2023 saa 4:00 Asubuhi na kufuatiwa na ufunguzi utakaofanyika saa 4:30 Asubuhi.** Waombaji wote mnakaribishwa kuhudhuria ufunguzi huo wa zabuni kwa gharama zenu.

Augustine Nyenza
Augustine Nyenza

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
NJOMBE